www.vpo.go.tz

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

MUUNGANO NA MAZINGIRA

TOLEO NA. 29

OKTOBA, 2019

# Samia: Dodoma ya kijani inawezekana



## NORWAY KUFADHILI MRADI WA REDD+



Jarida hili limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini | S.L.P 2502, Dodoma

Simu: +255 685 333 444

Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania

ofisi_ya_makamu_wa_rais

@vpo_tanzania





Scanned by CamScanner



# Samia: Dodoma ya kijani inawezekana

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema azma ya kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani iko pale pale.

Samia amesema hayo mara baada ya kutembelea shamba la miti lililopo katika eneo la Mzakwe katika Kambi ya Jeshi Makutupora Jijini Dodoma, ikiwa ni ufuatiliaji wa Kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani aliyozindua mwaka 2017 .

Makamu wa Rais ameupongeza uongozi wa Kambi ya Jeshi ya Makutupora, Wakala wa Misitu Tanzania na Watendaji wa Ofisi yake kwa kuhakikisha miti iliyopandwa mwezi Desemba 2017 inastawi.

"Vitabu vya dini vinasema moja kati ya sadaka endelevu ni kupanda miti, miti hii imekua na kustawi kwa sababu ya jitihada zenu za kuimwagilia na kuitunza, msikate tamaa.

"Endeleeni na kazi hii njema ambayo matokeo yake yanaonekana ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa mifumo ya hali ya hewa ambayo huimarisha shughuli za kilimo na maendeleo ya viwanda." alisisitiza Makamu wa Rais.

Nae Mkuu wa Kambi ya Jeshi ya Makutupora Luteni Kanali Festo Mbanga amesema kuwa miti 2300 ilipandwa Desemba 21, 2017 na kati ya hiyo miti 2076 imekua na kustawi ikiwa ni sawa na asilimia 90.3 ya miti yote iliyopandwa.

"Katika miti iliyooteshwa awali baadhi haikuota, hivyo tumefanya jitihada za kuirudishia, tumepanda takriban miti 300 ya ziada" alisema Luteni Kanali Mbanga.

Katika hatua nyingine Makamu wa Rais ameagiza Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuhakikisha tafiti zinakamilika mapema kutoka katika sampuli ya udongo iliyochukuliwa ili kubaini aina ya miti inayostawi katika eneo hilo na Jiji la Dodoma kwa ujumla.

Kampeni ya Kukijanisha Dodoma ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Desemba 21, 2017 katika eneo la Mzakwe Jijini Dodoma ambapo miti 2300 ilipandwa siku hiyo.



Scanned by CamScanner

# Norway kufadhili Mradi wa REDD+

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Norway nchini Bi Elisabeth Jacobsen.

Pamoja na masuala mbalimbali wamezungumzia namna ya kuendeleza ushirikiano katika miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ukiwemo wa Kupunguza Hewa ya Ukaa na Kupunguza Ukataji Miti (REDD+) wenye thamani ya Dola za Marekani 1,096,830 ambapo Serikali ya Tanzania na Norway zipo katika hatua za mwisho za mazungumzo ya kuingia makubaliano kwa ajili ya utekelezaji wake.

Akizungumza na Balozi huyo, Waziri Simbachawe alisema kutokana na umuhimu wa mazingira ipo haja ya kuwa na mtaala kwa shule zote maalumu kwa ajili ya kufundisha somo la mazingira kuanzia elimu ya msingi ili wanafunzi wawe na uelewa mkubwa wa sekta hiyo.

Alifafanua kuwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inasema kila taasisi inahusika katika shughuli zote za utunzaji na uhifadhi wa mazingira hivyo shule zinapaswa kufundisha wanafunzi ili wawe na uelewa juu ya dhana hiyo.

“Ipo haja ya kuwekeza kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi kwa kuwapa elimu ya mazingira ili kuwajengea uelewa, kuhusu sekta hiyo” alisisitiza Simbachawene.

Aidha Waziri huyo amezungumzia hatua mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Tanzania katika utunzaji wa mazingira kupitia Ofisi yake ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kwa ajili ya kupikia.

Alisema kuwa Ofisi yake iliwashindanisha wadau kutengeneza majiko mbadala ambayo hayatumii kuni na mkaa hivyo kusaidia kuepusha vitendo ya ukataji miti.

Katika hatua nyingine Balozi Jacobsen alipongeza Tanzania kwa utekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki na kusema hatua hiyo ni ya kuigwa na mataifa mengine ili kusaidia kuondosha madhara yanayotokana na matumizi ya mifuko hiyo.

Alishauri katazo hilo liendelee kuibua fursa za ajira kwa wananchi zikiwemo za kutengeneza mifuko mbadala na kusema kuwa ipo haja ya kufanya kazi kwa pamoja katika kuzuia uchafuzi wa mazingira katika bahari.





Scanned by CamScanner

# Makatibu Wakuu SADC waweka mikakati kukabili mabadiliko ya tabianchi




Makatibu Wakuu kutoka Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii wa nchi za SADC wamefanya vikao vya kujadili na kuweka agenda za mkutano wa Mawaziri wa sekta husika kutoka umoja huo.

Walijadili mpango mkakati wa pamoja wa kukabiliana na ujangili katika nchi wanachama na kuweka jitihada za pamoja za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumzia mkutano huo Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Malongo amesema, Mkutano wa Mawaziri wanaosimamia sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii utajadili masuala muhimu ikiwa ni pamoja na:- Mwenendo wa uridhiaji wa Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *Protocol on Environmental Management for Sustainable Development*.

Pia Mabadiliko ya Tabianchi; Kuundwa kwa Mkakati wa SADC wa Uchumi wa Bahari (SADC Strategy on Blue Economy); Mpango kazi wa SADC wa Kudhibiti Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (SADC Action Plan to Combat Desertification).

Aidha, Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa inayohusu Hifadhi ya Mazingira ambayo SADC ni mwanachama; Mikakati ya utafutaji wa fedha za kutekeleza masuala hifadhi ya mazingira na Hali na mwenendo wa utekelezaji wa sekta ya misitu, wanyamapori na utalii.

"Sote tunakubaliana kuwa bila Mazingira hakuna Maendeleo endelevu, tunaweka malengo ya kulinda rasilimali zetu kwa pamoja ambazo zinavuka mipaka mfano mito, misitu, maziwa" Malongo alisisitiza.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Profesa Adolf Mkenda alisema mkutano huo utajadili mambo mbalimbali ikiwemo vita dhidi ya ujangili ambayo inapaswa kuungwa mkono na nchi zote wanachama badala kuachwa kwa nchi moja moja.

"Tunahitaji kuwa na mpango mkakati wa kukuza utalii katika nchi za SADC hii ni moja kati ya ajenda muhimu zitakazojadiliwa" Alisema Profesa Mkenda.

Mkurugenzi wa Idara ya Chakula, Kilimo na Maliasili kutoka Sektretarieti ya SADC, Domingos Zephania Gove alisema kuwa wanahitaji kutembea pamoja kama nchi za SADC katika kuweka mikakati katika masuala ya kimazingira, Utalii na Wanyamapori. Gove alisema kuwa wanahitaji kuthibitisha programu za pamoja za kukuza utalii na kusimamia maliasili katika ukanda husika.



***Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Mhandisi Joseph Malongo akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kufunguliwa rasmi kwa Mkutano wa Makatibu Wakuu wa Wizara za Mazingira, Maliasili na Utalii kwa nchi za SADC.***



Scanned by CamScanner

# NEMC yafunga machinjio ya Msalato

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limefunga machinjio ndogo ya Msalato kwa muda usiojulikana na kupiga faini kwa kosa la kukithiri kwa uchafu wa mazingira na miundombinu chakavu.

Hatua hiyo imefikiwa mara baada ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kufanya ziara ya kushtukiza katika eneo hilo na kujionea Mazingira yasiyoridhisha kwa usalama wa afya za binadamu.

Katika ziara hiyo, wabunge wamejionea mazingira yasiyoridhisha na kuhatarisha afya za watumiaji wa nyama inayochinjwa machinjioni hapo ikiwa ni pamoja na kurundikana kwa samadi, kukithiri kwa harufu kali na kukosekana kwa maji safi.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Mussa Sima amesema lazima hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa manufaa ya afya za walaji. “Sisi watu wa Mazingira afya za binadamu ni kipaumbele namba moja, hali hii haikubaliki” Sima alisisitiza.

Sima amemuagiza Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Nchini (NEMC) Dkt. Samwel Gwamaka kufanya tathmini ya haraka na kina na kuhakikisha kuwa machinjio yanazingatia taratibu zilizopo katika Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.



***Sehemu ya jengo la machinjio ndogo ya Msalato jijini Dodoma ambayo imefungwa na Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kutokana na mazingira yasiyoridhisha.***

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira Kanali Mstaafu Masoud Ali amesema hali ya usafi katika machinjio hiyo haidhirishi na kuwataka NEMC kuchukua hatua.

“NEMC msingechukua hatua, sisi Kamati tungechukua, haiwezekani hali hii haikubaliki” Alisisitiza Mhe. Masoud Ali.

Wakati huo huo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC amelitoza faini Jiji la Dodoma ya kiasi cha Shilingi Milioni tano (5) kwa mujibu wa kifungu namba 194 cha sheria ya usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na kutakiwa kuilipa ndani ya wiki mbili.

Aidha, Afisa Mifugo wa Jiji la Dodoma Bw. Gratius Mwesiga alieleza Kamati hiyo kuwa ukarabati katika eneo hilo umeanza na unaendelea kwa awamu, ikiwa ni pamoja na ukarabati wa mifumo ya maji taka.



***Wabunge wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira wakiwa katika ziara ya kushtukiza eneo hilo na kujionea mazingira yasiyoridhisha kwa usalama wa afya za binadamu.***



Scanned by CamScanner

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akifungua Kikao cha Mawaziri wa Jumuia ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC) wa Sekta ya Mazingira, Maliasili na Utalii Jijini Arusha.*



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Mussa Sima (wa pili kulia) akibadilishana mawazo na Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangalla katika viwanja vya Ukumbi wa AICC jijini Arusha kabla ya kuanza kwa kikao cha Mawaziri wa SADC.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Menejimenti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira katika kikao kazi kilichojadili Utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais Jijini Dodoma.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Rais Edgar Lungu wa Zambia wakati wa Hafla ya kuapishwa Rais Mpya wa Botswana Dkt. Mokgweetsi E, K, Masisi iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Botswana Indoor Arena Makamu wa Rais alimuwakilisha Rais Dkt. John Pombe Magufuli Kwenye Hafla hiyo.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene akizindua kitabu kinachozungumzia mabadiliko ya tabianchi kilichoandikwa na wataalamu kutoka Tanzania, Norway na Marekani.*



*Washiriki wa Mkutano wa Mawaziri wa Mazingira, Maliasili na Utalii wa nchi za SADC wakitembelea vivutio vya utalii vikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Arusha (ANAPA).*



Scanned by CamScanner



# Miradi, Programu za maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano zanufaisha wengi

Idara ya Muungano chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais hivi karibuni imewakutanisha Waratibu wa miradi na programu za maendeleo zinazofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mgeni rasmi katika kikao kazi hicho Mhasibu Mkuu Bw. Paschal Karomba alisema kikao hicho kilijikita katika mambo makuu mawili, kupata taarifa ya utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo na kukubaliana namna bora ya upatikanaji wa taarifa za utekelezaji.

Miradi na programu zinazoendelea kutekelezwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund – TASAF III ); Mradi wa Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga (*Expanded Rice Production Project – ERPP).*

Pia Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Maeneo ya Pwani- LDCF; Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA).

Aidha, Programu nyingine ni Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani na Huduma za Fedha Vijijini *(Market Infrastracture, Value Addition and Rural Finance - MIVARF)*; Mradi wa Udhibiti wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – SWIOFISH.

Pia Mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania na Mradi wa Uboreshaji wa Elimu kupitia *Global Partnership for Education,* pamoja na T*anzania Initiatives for Preventing Aflatoxin Contamination – TANIPAC na Public Financial Management Reform Programe – PFMRP*





Scanned by CamScanner



# Serikali yatekeleza Mradi kuwezesha taasisi kusimamia kemikali, taka

Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa kemikali na taka nchini.

Mradi huu una thamani ya Dola za Kimarekani 235,000 ambapo unafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEP) kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lengo la mradi ni kuwezesha Taasisi kutunga, kusimamia na kutekeleza Sera na Kanuni katika Usimamizi wa Kemikali na Taka.

Mradi huu umetoa mafunzo kwa Mamlaka za udhibiti katika sekta ya mafuta na gesi.

Jumla ya maafisa 105 kutoka Mamlaka za udhibiti walipewa mafunzo.

Pia mafunzo kwa maafisa 52 wa Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa kemikali na taka.

**Kazi zilizofanyika;**

- Kuandaa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa zebaki.
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa kemikali na taka nchini.
- Kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 125 kuhusu usimamizi wa kemikali na taka katika sekta ya kilimo.
- Kufanya tathmini ya uwezo wa kitaasisi katika usimamizi wa kemikali na taka nchini.
- Kuandaa kanzi data ya Kitaifa ya kemikali na taka.
- Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Kemikali na Taka.
- Kuandaa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa zebaki ambazo ziko katika hatua ya mwisho ya kukamilishwa.

Aidha, jumla ya maafisa 282 kutoka mamlaka za udhibiti, sekta ya kilimo na Serikali za Mitaa wamepatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa kemikali na taka.

***Kazi zingine zilizofanyika***

Kuandaa kanzidata ya kitaifa ya kemikali na taka uko hatua za awali katika hatua ya pili ya rasimu.

Madhara yatokanayo na usimamizi wa kemikali na taka usio madhubuti hayaathiri tu afya na mazingira ya eneo husika, bali huathiri dunia nzima kipindi hadi kipindi.

Kwa muktadha huo, ni wajibu wa kila mmoja wetu kutumia kemikali kwa usahihi na kuchukua hatua stahiki za kuepuka madhara yatokanayo na kemikali na taka zake.



Scanned by CamScanner

# Simbachawene: Mwalimu Nyerere alikuwa mwanamazingira wa kweli

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. George Simbachawene amesema Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere alikuwa ni mtunzaji mkubwa wa mazingira ingawa katika enzi za uhai wake suala la mabadiliko ya tabianchi halikuwa changamoto kubwa katika Taifa letu wala ajenda ya ulimwengu kama ilivyo leo.



Simbachawene alitoa kauli hiyo wakati akifungua Kongamano la Kimataifa la Mabadiliko ya Tabianchi lililofanyika katika Ukumbi wa Mwalimu Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa mabadiliko ya tabianchi ni ajenda ya dunia na kwa mantiki hiyo Serikali haina budi kuanza kutoa elimu ya kukabiliana na madhara yatokanayo na changamoto hiyo.

Alisema kuwa Mwalimu Nyerere alikuwa mtaalamu na mtunzaji wa mazingira ambaye alichochea maendeleo endelevu kwa mfano alizungumzia sheria ya kuhifadhi maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na Hifadhi za Taifa.

Aidha, waziri huyo alisema kuwa shughuli za kibinadamu zimekuwa zikisababisha ongezeko la hewa ukaa na kuleta joto kubwa sambamba na mabadiliko ya majira hivyo elimu ikitolewa kwa wananchi italeta tija katika dhana nzima ya utunzaji wa mazingira.

# Tanzania kushawishi nchi za SADC kupiga marufuku mifuko ya plastiki

Wataalamu wa Mazingira kutoka nchini Tanzania walioshiriki katika mkutano wa Mawaziri wa Mazingira, Maliasili na Utalii wa SADC wameanza juhudi za kuzishawishi nchi wanachama wa SADC kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ili kudhibiti uharibifu wa mazingira katika ukanda huo.

Akizungumza mara baada ya kuhudhuria mkutano wa wataalamu wa maandalizi ya mkutano wa Mawaziri wa Mazingira, Maliasili na Utalii wa SADC, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Kemilembe Mutasa (pichani) alisema katika mkutano huo wamekuwa wakizishawishi nchi wanachama kuridhia itifaki ya hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo.

Kwa upande wake Afisa Mazingira Mkuu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Cletus Shengena alisema wataalamu wa mazingira kutoka nchi za SADC wamekuwa na mikutano ya kuweka mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo ni changamoto kubwa inayokabili nchi wanachama Tanzania ikiwa ni nchi mojawapo.

Shengena alisema mkakati huo utawasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari zinazojitokeza ikiwemo mafuriko na upepo mkali na vimbunga katika nchi wanachama.

Pia Afisa Mazingira Mkuu Bi. Emelda Teikwa Adam alisema wameangazia fursa za kukuza uchumi wa nchi za SADC kwa kutumia uchumi wa bluu unaojulikana kama uchumi wa bahari unaotumika kwa njia ya usafirishaji, uvuvi na kutoa nishati kwa maana ya uchimbaji wa mafuta na gesi kama njia za kukuza uchumi wa nchi za SADC.



Emelda anasema kuwa ili uchumi huo uwe endelevu mazingira yanapaswa kutunzwa na kulindwa ili wananchi waweze kunufaika na fursa za uchumi wa bluu ambao ukitumika vizuri unaweza kupunguza umaskini.



Scanned by CamScanner

# Waliokiuka maagizo ya Serikali kufutiwa vibali vya taka hatarishi



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. George Simbachawene ameagiza kufutwa kwa vibali vya wafanyabiashara wote wanaosafirsha vyuma chakavu ambao hawakufuata maelekezo na maagizo ya Serikali.

Alisema hayo jijini Dodoma wakati wa mkutano wa kupokea ripoti ya kamati aliyoiunda kwa ajili ya uchunguzi wa makontena ya bidhaa za chuma chakavu yaliyokuwa yamekamatwa kwa uchunguzi katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Ninaagiza wafanyabiashara wote waliokiuka maagizo na maelekezo ya Serikali wafutiwe vibali vyao,'

Waziri Simbachawene aliipongeza kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya na amepokea mapendekezo yote yaliyopendekezwa na kamati hiyo.

"Nawapongeza sana mmefanya kazi kubwa na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati nimeyapokea na ninaagiza NEMC kama msimamizi mkuu kusimamia jambo hili"alisema Waziri Simbachawene.

Aliongeza kuwa wafanyabiashara wa vyuma chakavu siyo wakweli kwani wengi wao wanasafirisha bidhaa zingine tofauti na vyuma chakavu huku wakisingizia kuwa wamebeba vyuma chakavu wakati siyo kweli.

"Vitu mbalimbali vinasafirishwa kama vile mifuniko ya chemba, injini za vifaa vya moto, mita za maji, vipande vya bomba na vingine ni vipya kabisa na haviko kwenye kundi la vyuma chakavu," alidokeza.

Akiongea wakati wa kumkaribisha Simbachawene Mkuu wa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka alisema kuwa ziko kampuni sita ambazo makontena yao yalikamatwa bandarini na yalikuwa yakifanyiwa uchunguzi.

Makampuni hayo ni J. M Kambi and General Services (makontena 88), JBR Group of Companies (makontena 35), Villa Plast Ltd (makontena 3) , Three Star Metal Group (makontena 12) na Steel Com Ltd (makontena 2).

Waziri Simbachawene alifanya ukaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na kuagiza makontena yote ya kampuni tajwa hapo juu yaliyokua yamebeba shehena ya vyuma chakavu kuzuiliwa kusafirisha bidhaa hizo na kufanyike uchunguzi wa haraka.



Scanned by CamScanner



# Dola Mil 5.7 kunufaisha wakazi ZIWA NYASA

Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu utekelezaji wa mradi wa Usimamizi endelevu wa matumizi ya ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa.

Huu ni mradi unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (GEF) kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Hifadhi ya Mazingira (UNEP) kwa Dola za Kimarekani 5,748,980.

Bonde la Ziwa Nyasa ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa watu takribani zaidi ya Milioni moja wanaoishi kwenye Bonde la Ziwa hili.

Ziwa hilo lina aina mbalimbali za bioanuai wakiwemo za samaki ambao hawapatikani sehemu nyingine duniani.

Hata hivyo, bioanuai hizo zinatishiwa kutoweka kutokana na matumizi yasiyo endelevu katika bonde hilo. Eneo la bonde hilo linakabiliwa na changamoto mbalimbali za kimazingira.

Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa misitu unaosababishwa na kilimo kisicho endelevu, ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa na uchomaji moto ovyo.

Zingine ni uvuvi usio endelevu na mmomonyoko wa udongo katika maeneo ya miinuko inayozunguka Ziwa Nyasa, uchimbaji holela wa madini na kutoweka kwa baadhi ya viumbe wa majini hasa samaki.

***Malengo ya Mradi***

Mradi huu unalenga kukuza uwezo wa usimamizi na matumizi endelevu ya Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa, kukabiliana na uharibifu wa mazingira katika bonde la ziwa hilo ambao unatokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu.

Pia malengo mengine ni kuboresha maisha ya jamii ambayo inazunguka bonde na mwambao wa Ziwa Nyasa pamoja na kuboresha matumizi na usimamizi wa maliasili zilizopo hapo.

Shughuli za mradi ni kujenga uwezo wa uhifadhi wa mazingira katika bonde la Ziwa Nyasa kwa kubaini na kufanya tathmini ya shughuli za matumizi ya ardhi katika wilaya zilizokusudiwa.

Aidha, shughuli nyingine ni kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi katika bonde hilo, kuelimisha na kukuza uelewa kuhusu mbinu bora na endelevu za usimamizi wa ardhi na kujenga uwezo na kuimarisha Halmashauri zote za Wilaya zilizopo katika bonde hilo.

Kuwa na mifumo jumuishi ya usimamizi katika bonde kwa kutumia mbinu endelevu za usimamizi ardhi, kufundisha kilimo endelevu kinachohifadhi mazingira na maeneo ya Ziwa yaliyoharibiwa na vyanzo vya maji yanakarabatiwa na kuhifadhiwa.

Malengo mengine pamoja na mbinu za kilimo bora cha hifadhi ardhi inayofaa kwa kilimo, kubainishwa na kutekelezwa njia mbadala ya kuongeza kipato.

Maeneo yaliyotelekezwa kutokana na shughuli za uchimbaji kukarabatiwa kwa kupandwa miti na kuendeleza mbinu za asili za kuhifadhi ardhi na mazao ya chakula.

Matokeo chanya yatakayotokana na utekelezaji wa mradi yatasambazwa na kuendelezwa katika sehemu zingine zenye changamoto zinazofanana na za maeneo ya bonde la Ziwa Nyasa.

Utekelezaji wa Mradi huu ulianza Januari, 2018 katika mikoa ya Ruvuma (Mbinga na Nyasa), Mbeya (Kyela) na Njombe (Ludewa na Makete).

Wadau wengine wanaoshiriki kutekeleza mradi huu ni pamoja na Tume ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi, Chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine (SUA); Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.



Scanned by CamScanner

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa Wakala wa Misitu Tanzania Kanda ya Kati Bi. Teddy Yoramu kuhusu ukuaji wa miti iliyopandwa katika eneo la Mzakwe jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima akizungumza na mtangazaji wa kituo cha televisheni cha Clouds Bw. Hassan Ngoma kabla ya ufunguzi wa Mkutano wa UMawaziri wa sekta za Mazingira, Malisiali na Utalii wa nchi za SADC jijini Arusha.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri jijini Dodoma hivi karibuni.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. George Simbachawene akizungumza katika kikao na ujumbe kutoka Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) kujadili kuhusu Mradi wa kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI kilichofanyika jijini Dodoma.*



*Wabunge wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira walipotembelea machinjio ndogo ya Msalato na kujiona hali mbaya ya mazingira katika eneo hilo. Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC imefunga machinjio hiyo na kupiga faini Jiji la Dodoma ya kiasi cha Shilingi Milioni 5.*





Scanned by CamScanner

# Ofisi ya Makamu wa Rais, Wizara ya Viwanda zakutanisha wadau wa mifuko mbadala



*Mkurugenzi wa Idara ya Viwanda toka Wizara ya Viwanda na Biashara Bw. Leo Lyayuka akifungua kikao cha wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa mifuko mbadala wa plastiki, kilichofanyika katika ukumbi wa JNICC jijini Dar es Salaam.*

Zoezi la upigaji marufuku mifuko ya plastiki limefanikiwa kwa kiasi kikubwa na kufanyika kwa weledi hatua iliyoondoa na malalamiko yoyote kutoka kwa wananchi.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Viwanda toka Wizara ya Viwanda na Biashara Bw. Leo Lyayuka wakati akifungua kikao kilichoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara hiyo kilichowakutanisha wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa mifuko mbadala wa plastiki kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Bw. Lyayuka alisema lengo la kikao hiko ni kusikiliza hoja na changamoto mbalimbali kutoka kwa Wazalishaji, Wauzaji na Wasambazaji wa mifuko hiyo, na hivyo basi kuwezesha Serikali kuzipatia changamoto hizo uvumbuzi.

"Kwenye mafanikio yoyote hapakosi changamoto, vivyo hivyo kwenye zoezi hili tumepata mafanikio makubwa lakini kuna changamoto ambazo zimejitokeza na kama zisipotafutiwa ufumbuzi wa haraka zitaharibu na kurudisha nyuma mafanikio makubwa yaliyopatikana.

Kwa hiyo kikao chetu kitajikita katika kuzibaini changamoto zote na kupendekeza mapendekezo namna ya kuzitatua," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Bi Kemilembe Mutasa alisema kuwa kikao hiko kina lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki, kuibua changamoto za utekelezaji na namna ya kukabiliana nazo.

Bi. Kemi alizitaja changamoto kuwa zipo katika viwango vya ubora vinavyotakiwa vya mifuko mbadala, hali ya uzalishaji na usambazaji wa mifuko mbadala, uzalishaji na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya mifuko mbadala wa plastiki.

Mkurugenzi msaidizi huyo aliongeza kuwa viwango vya ubora wa mifuko mbadala na Changamoto zina zojitoke za katika uzalishaji wa mifuko mbadala wa plastiki.

Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikiandaa vikao kama hivyo mara nyingi ili kuweza kupata maoni na changamoto juu ya uzalishaji, usambazaji na biashara ya mifuko mbadala wa plastiki kwa pamoja.



*Mgeni Rasmi katika kikao cha wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa mifuko mbadala kilichoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Viwanda na Biashara Bw. Leo Lyayuka akiwa katika picha ya pamoja na Washiriki waliohudhuria kikao hiko katika Ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere (JNICC)*



Scanned by CamScanner

# Ofisi ya Makamu wa Rais yakutana na Kamati ya Bunge ya Mazingira

Sera ya Usimamizi wa Mazingira (1997) na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.20 ya mwaka 2004 (Sura ya 191) ndio muundo muhimu wa usimamizi wa mazingira nchini.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mussa Sima mara baada ya kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango wa pili wa Maendeleo wa miaka mitano katika Sekta ya Mazingira mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira jijini Dodoma.

Naibu Waziri Sima alisema katika kuhusisha masuala ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali, Ofisi yake imeandaa Sera, Sheria na Mikakati inayohusiana na uhifadhi wa Rasilimali za Misitu, vyanzo vya Maji, Ardhi oevu, Wanyamapori, Gesi asilia, Madini na Nishati.

Mambo mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na kuongoa mifumo ikolojia ya majini iliyoharibika ili kuwepo kwa huduma bora kwa afya ya jamii na ikolojia; kuhifadhi rasilimali za bahari kwa maendeleo endelevu, Miradi na kampeni mbalimbali zimetekelezwa zikilenga kupunguza uharibifu wa ardhi kwa maendeleo endelevu.

Aidha katika kuimarisha mifumo ya kijamii ya usimamizi wa rasilimali, Naibu Waziri Sima alisema Ofisi yake imeimarisha usimamizi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya nchi kupitia Mradi wa Bonde la Ziwa Nyasa, Mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika, Mradi wa usimamizi endelevu wa ardhi, ambayo yote inasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa miradi mbalimbali na kukuza teknolojia za nishati jadidifu

(biogas, petroli gesi (LPG), nishati ya jua, pepo na joto la ardhi pamoja na kusaidia programu za utafiti, kukuza teknolojia mpya, mbegu bora, udhibiti wa wadudu waharibifu, na mbinu bora za kilimo.

Wakichangia wasilisho hilo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Mhe. Suleiman Saddiq na Kanali Mstaafu Masoud Ali walishauri Serikali kuwa na mikakati thabiti ya kuzuia uharibifu wa mazingira nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi katika kutunza rasilimali za misitu, ardhi na mazingira yanayowazunguka kwa kushirikiana na wakaguzi wa Mazingira.

Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipokea taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu utekelezaji wa wa Mpango wa miaka mitano wa Maendeleo kwa Sekta ya Mazingira (Mafanikio na changamoto) pamoja na Ripoti ya hali ya mazingira nchini.



*Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na na Mazingira wakiwa katika kikao cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa miaka mitano katika Sekta ya Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais jijini Dodoma.*



Scanned by CamScanner



## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

**Anwani ya simu:** "MAKAMU"
**Simu Na.:** +255 26 2329006
**Fax Na:** +255 26 2329007
**Barua Pepe:** km@vpo.go.tz

Mji wa Serikali
Eneo la Mtumba,
Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais.
Ihumwa, S.L.P 2502
DODOMA, TANZANIA

**Dodoma, Novemba 04, 2019**

## TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kusimamia marufuku ya katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki kwa kushirikiana na Kikosi kazi cha Kitaifa. Kwa siku za hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la uzalishaji, utengezaji na uingizaji na usambazaji wa mifuko isiyokidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Kikosi kazi cha Kitaifa cha kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki pamoja na Kamati za Mikoa na Wilaya wanaendesha oparesheni maalumu nchi nzima kwa lengo la kusaka mifuko isiyokidhi viwango.

Tarehe 30/10/2019 NEMC ilikamata marobota 21 katika Wilaya ya Misenyi, Mkoani Kagera na marobota 7 Mkoani Arusha ambayo yanashikiliwa katika kituo cha polisi cha Arusha. Upelelezi wa mashauri haya bado unaendelea.

Leo tarehe 4/11/2019 Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi kwa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza wamekamata shehena ya mifuko isiyokidhi viwango gunia 8 yenye thamani ya Shilingi 10,000,000/- Mifuko hiyo iliingia kupitia bandari bubu ya Bwiru jijini Mwanza ikitokea nchi jirani. Watuhumiwa watafikishwa mahakamani na mifuko hiyo itateketezwa kwa mujibu wa sheria kama itakavyoelekezwa na NEMC.

Ofisi ya Makamu wa Rais, inatoa wito kwa wafanyabiashara wote wanaojihusisha na uingizaji, usambazaji na uuzaji wa mifuko mbadala kuhakikisha wanazingatia matakwa ya Sheria. Aidha, wafanyabiashara wanasisitizwa kuacha kuzalisha, kuingiza nchini, kuuza na kusambaza mifuko isiyokidhi viwango. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya wote wanaokiuka agizo hilo.

**Imetolewa na**
**Lulu Mussa**
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

## TAARIFA KWA UMMA

Ofisi ya Makamu wa Rais ilianza kutekeleza azimio la Serikali la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 1 Juni 2019. Tunashukuru umma wa Watanzania kwa kuitikia vyema utekelezaji wa katazo hili.

Hata hivyo, kumeanza kujitokeza uvunjifu wa sheria katika uzalishaji na uingizaji wa mifuko mbadala aina ya *non-woven*. Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeweka vigezo vya mifuko mbadala aina ya *non-woven* inayoweza kutumika nchini. Vigezo hivyo ni pamoja na:

1. Uzito usiopungua GSM 70 (Gram per Square Metre)
2. Iwe inaweza kurejelezwa (Recyclable)
3. Ioneshe uwezo wa kubeba (Carrying capacity)
4. Iwe imethibishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

Baadhi ya wafanyabishara wasio waaminifu wamekuwa wakiingiza/kuzalisha mifuko mbadala aina ya *non-woven* ambayo haikidhi vigezo tajwa.

Aidha, kumekuwa na matumizi yasiyokubalika ya mifuko myepesi na laini aina ya *"Tubings"* kubebea bidhaa. Agizo ni kwamba, mifuko hii inapaswa kutumika kama vifungashio vya bidhaa maalumu na viwe na lakiri (*seal*) ili kuzuia kuongeza bidhaa nyingine katika kifungashio hicho.

Kwa siku za hivi karibuni mifuko hii laini imekuwa ikitumika kama vibebeo jambo ambalo ni kosa kisheria. Hatua ya kuongezeka kwa matumizi yasiyo sahihi ya mifuko tajwa inaanza kuleta athari katika mazingira.

Kikosi Kazi cha Taifa cha kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Kamati za Mikoa/Wilaya wataendesha operesheni kabambe nchi nzima ili kubaini wanaovunja matakwa ya katazo hili ikiwemo watumiaji na wazalishaji wa mifuko mbadala aina ya *non-woven* isiyokidhi viwango, pamoja na matumizi ya *''tubings"*.

Kumbuka, Mazingira ndiyo yanayolea uchumi wa Taifa letu, hivyo anayeharibu mazingira ni sawa na mhujumu uchumi. Kwa muktadha huo watakaobainika kuvunja Sheria watakachukuliwa hatua stahiki.

Tunaendelea kuushukuru umma wa Watanzania kwa kutekeleza agizo hili na kutunza Mazingira kwa ustawi wa Taifa letu.

Kwa maelezo na ufafanuzi kuhusu suala hili au masuala yoyote yanayohusu mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa **namba maalumu za simu kwa ajili hiyo**. Mwananchi hataingia gharama kupiga simu katika namba hizi ambazo zinapatikana masaa 24, wasiliana nasi kwa kutuma ujumbe mfupi (SMS) au ujumbe wa Whatsapp kupitia:

| KUPIGA BILA MALIPO | SMS/WHATSAPP |
|---|---|
| (0800 110 115) | +255 737 796 253 |
| (0800 110 116) | +255 737 796 252 |
| (0800 110 117) | +255 737 796 249 |
| (0800 110 118) | +255 737 796 250 |

**Imetolewa na**

**Mhandisi Joseph K. Malongo**
**KATIBU MKUU**
04/11/2019



Scanned by CamScanner









Limetolewa na Kitengo cha Mawasiliano
Serikalini Ofisi ya Makamu wa Rais
S.L.P. 2502, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 266 235 2038
Nukushi +266 235 0002
Barua pepe: ps@vpo.go.tz
Tovuti: www.vpo.go.tz
Facebook: Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania
Simu ya mkononi: 0685 333 444
Instagram: ofisi_ya_makamu_wa_rais
Twitter: @vpo_tanzania

Scanned by CamScanner